Hotuba ya Kwanza.

**DINI NI NYEPESI**

**WEPESI KATIKA IBADA NA USAMEHEVU KATIKA MASHIRIKIANO**


**Imefasiriwa**

**Na**

**Profesa/Ayman Ibrahim Alasar**

**Kitivo cha lugha na ufasiri**


Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe, Msemaji ndani ya Kitabu chake Kitukufu: يُرِيدُ اللهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلاَ يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ {**Mwenyezi Mungu anawatakia wepesi wala hawatakii uzito**}.

Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad S.A.W ni mja wake na Mtume wake, ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma amani na baraka kwake pamoja na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wanaomfuata kwa uzuri mpaka siku ya malipo.

**Baada ya Utangulizi**:

Kwa hakika sura za utukufu katika dini yetu ni nyingi zisizo hesabika, na yaliyo na sura ya pekee zaidi kwenye dini ya Kiislamu ni swala zima la wepesi na usamehevu, kwani dini yetu yote ni uadilifu, huruma, wepesi, usamehevu na ubinadamu, na kila chenye kufikia kwenye malengo haya makubwa hilo lipo kwenye mfumo wa Uislamu, na kila lenye kugongana na hayo kwa hakika yanapingana na Uislamu pamoja na malengo yake na makusudio yake, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

**وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ مِلَّةَ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ هُوَ سَمَّاكُمُ الْمُسْلِمِينَ مِن قَبْلُ وَفِي هَذَا لِيَكُونَ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ.**

{**Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini. Nayo ni mila ya baba yenu Ibrahim. Yeye (Mwenyezi Mungu) alikuiteni Waislamu tangu zamani, na katika hii (Qurani) pia, ili awe Mtume shahidi juu yenu, na nyinyi muwe mashahidi kwa watu**}. Na Mwenyezi Mungu Anasema tena: **لا يُكَلِّفُ اللهُ نَفْسًا إِلا وُسْعَهَا** {**Mwenyezi Mungu hailazimishi nafsi ya mwanadamu isipokuwa kwa lile iwezalo**}. Na Mtume S.A.W amesema:

**إِنَّ الدِّينَ يُسْرٌ، وَلَنْ يُشَادَّ الدِّينَ أَحَدٌ إِلَّا غَلَبَهُ، فَسَدِّدُوا وَقَارِبُوا وَاسْتَعِينُوا بِالْغَدْوَةِ وَالرَّوْحَةِ وَشَيْءٍ مِنَ الدُّلجَةِ.**

"***Hakika dini ni nyepesi, hakuna atakayeifanyia uzito isipokuwa itamshinda, basi ikusudieni ukati na kati katika ibada, na ikaribieni katika hilo, na takeni msaada wa kutekeleza hayo nyakati za asubuhi jioni na alfajiri***". Na Mtume S.A.W akasema tena: **إِنَّ خَيْرَ دِينِكُمْ أيسَرُهُ** "***Hakika ubora wa dini yenu ni wepesi***". Na akasema tena S.A.W: **إنَّ اللهَ رضِيَ لهذه الأمةِ اليُسرَ، وكرِه لهم العُسرَ** "***Hakika Mwenyezi Mungu ameridhia kwa Umma huu wepesi, na amechukia kwao kufanyia uzito***". Akaendelea tena kusema: **إِنِّي بُعثتُ بالحنيفيَّةِ السَّمحَةِ** "***Hakika nimeletwa kwa misingi ya ukati na kati ya usamehevu***".

Mwenye kuzingatia maisha ya Mtume S.A.W atafahamu kwa yakini kuwa alikuwa amezungukwa na mfano bora kwa umma wake na wanadamu wote katika usamehevu na wepesi, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema kupitia ulimi wa Mtume wetu S.A.W: **قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُتَكَلِّفِينَ** {**Sema (Ewe Mtume) Sikuombeni malipo juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu**}. Na Mtume S.A.W anasema: **إِنَّ اللَّهَ لم يَبْعَثْنِي مُعَنِّتًا، ولا مُتَعَنِّتًا، وَلَكِنْ بَعَثَنِي مُعَلِّمًا مُيَسِّرًا** "***Hakika Mwenyezi Mungu hakunileta kuwa mwenye kuleta ugumu wala msimamo mkali, bali amenileta kuwa mwalimu mrahisishaji***". Na Bi Aisha R.A anasema:

**مَا خُيِّرَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَيْنَ أَمْرَيْنِ إِلَّا أَخَذَ أَيْسَرَهُمَا مَا لَمْ يَكُنْ إِثمًا، فَإِنْ كَانَ إِثمًا كَانَ أَبْعَدَ النَّاسِ مِنْهُ.**

"***Mtume S.A.W hakupewa hiyari kati ya mambo mawili isipokuwa huchukuwa lililojepesi zaidi, ikiwa jambo la dhambi basi alikuwa ni mtu wa kuwa mbali nalo sana***". Na Mtume S.A.W anasema:

**إِنِّي لأَدْخُلُ فِي الصَّلاَةِ وَأَنَا أُرِيدُ إِطَالَتَهَا، فَأَسْمَعُ بُكَاءَ الصَّبِيِّ فَأَتَجَوَّزُ فِي صَلاَتِي؛ مِمَّا أَعْلَمُ مِنْ شِدَّةِ وَجْدِ أُمِّهِ مِنْ بُكَائِه.**

"***Hakika ninapoingia kwenye swala na ninataka kurefusha, nikasikia sauti ya mtoto analia basi ninafupisha swala yangu, kwani ninafahamu shida anayopata mama yake kutokana na kulia kwake***".

Usamehevu na wepesi katika dini yetu ya kati na kati ni mfumo kamili uliochukuwa nafasi, kwa upande wa ibada ya swala Mtume wetu Muhammad S.A.W anasema:

**يا أَيُّهَا النَّاسُ، إنَّ مِنكُم مُنَفِّرِينَ، فمَن أَمَّ النَّاسَ فَلْيَتَجَوَّزْ، فإنَّ خَلْفَهُ الضَّعِيفَ والكَبِيرَ وذَا الحَاجَةِ.**

"***Enyi watu, hakika miongoni mwenu wapo wenye kuwashawashi watu kuchukia swala, hivyo mwenye kuwaswalisha watu basi asirefushe, kwani nyuma yake kuna watu wagonjwa watu wazima kwa umri na watu wenye mahitaji mbalimbali***". Na Mtume S.A.W alimuelekeza Amrana Ibn Haswin R.A pindi alipokuwa anaumwa akamuambia: "*Swali ukiwa umesimama, ikiwa huwezi swali ukiwa umekaa, ikiwa huwezi basi swali ukiwa umelala ubavu*". Miongoni mwa wepesi katika ibada ni pamoja na ruhusa ya kula mchana wa Ramadhani wakati wa safari, na katika wepesi na usamehevu katika ibada ya hija ni kusaidiwa watu wasiojiweza katika urushaji wa vijiwe, na kurefushwa muda wake, na kufaa kuwakilishwa katika urushaji kwa wale wasioweza kutekeleza wenyewe, kwani Mtume wetu S.A.W hajafanya wepesi wa kitu zaidi ya kuwepesisha kwa mahujaji wa Nyumba ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kauli yake maarufu: **افْعَلْ وَلا حَرَج** "***Fanya hakuna ubaya***".

****

**Hotuba ya pili**:

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimuendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume wetu Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Hakuna shaka kuwa Sharia ya Kiislamu imekuwa na sifa ya wepesi na usamehevu kwa upande wa mashirikiano pia, kwani umeondoa uzito na tabu kwa watu katika maswala ya kuuziana na kununua, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ إلا أَنْ تَكُونَ تِجَارَةً عَنْ تَرَاضٍ مِنْكُمْ ولا تَقْتُلُوا أَنفُسَكُمْ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا.**

{**Enyi mlio amini! Msiliane mali yenu kwa dhulma, isipokuwa iwe biashara kwa kuridhiana wenyewe. Wala msijiuwe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwarehemu**}. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amendelea kusema:

**وَإِنْ كَانَ ذُو عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ إِلَى مَيْسَرَةٍ وَأَنْ تَصَدَّقُوا خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ.**

{**Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai) angoje mpaka afarijike. Na mkilifanya deni kuwa ni sadaka, basi ni bora kwenu, ikiwa mnajua**}. Na Mtume S.A.W amesema: **رَحِمَ اللَّهُ رَجُلًا سَمْحًا إِذَا بَاعَ، وَإِذَا اشْتَرَى، وَإِذَا اقْتَضَى** "***Mwenyezi Mungu humfanyia huruma mtu mwenye kusamehe pindi anapouza na anaponunua na anapo dai haki***".

Usamehevu katika kuuza kunahitaji muuzaji kutokuweka faida kubwa sana, au kufanya ukiritimba wa bidhaa yake, au kupunguza uzito wa mizani yake, au kutumia vibaya matatizo ya watu, kama vile inapelekea kwa mnunuzi kuwa ni mtu msamehevu kwa muuzaji, kwani asiwe mwenye kuwapunguzia watu vitu vyao, na usamehevu katika kutaka haki, ina maanisha mtu kutaka haki yake au deni lake kwa upole na wepesi pamoja na usamehevu.

Kwani Mtume wetu S.A.W ametueleza kuwa wepesi na usamehevu katika mashirikiano ni miongoni mwa sababu za kuwokoka siku ya Kiyama, ambapo Mtume wetu S.A.W anasema:

**حُوسِبَ رَجُلٌ مِمَّنْ كَانَ قَبْلَكُمْ، فَلَمْ يُوجَدْ لَهُ مِنَ الْخَيْرِ شَيْءٌ، إِلَّا أَنَّهُ كَانَ يُخَالِطُ النَّاسَ، وَكَانَ مُوسِرًا، فَكَانَ يَأْمُرُ غِلْمَانَهُ أَنْ يَتَجَاوَزُوا عَنِ الْمُعْسِرِ، قَالَ: قَالَ اللهُ عَزَّ وَجَلَّ: نَحْنُ أَحَقُّ بِذَلِكَ مِنْهُ، تَجَاوَزُوا عَنْهُ.**

"***Kuna mtu alikuwa kabla yenu, hakuwa na matendo mema hata kidogo, isipokuwa alikuwa akiishi vizuri na watu, na alikuwa akiwafanyia watu wepesi, kwani alikuwa akimuamrisha mtoto wake kuwasamehe wasio na uwezo, akasema: Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: Sisi ndio wenye haki zaidi kuliko yeye, tumemsamehe***". Na anasema S.A.W:

**مَنْ أَنْظَرَ مُعْسِرًا أَوْ وَضَعَ عَنْهُ أَظَلَّهُ اللهُ فِي ظِلِّهِ يَوْمَ لَا ظِلَّ إِلَّا ظِلُّهُ.**

"***Mwenye kumuangalia mtu aliyekuwa na uzito au akamuondolea tatizo lake, Mwenyezi Mungu atamfunika katika kivuli chake siku isiyo na kivuli isipokuwa kivuli chake***". Hivi ndio usamehevu katika mambo mengine ya mashirikiano na watu wote, kwa upande wa kuuza na kununua kulipa na kutaka malipo kuishi pamoja na kumkubali mwengine.

Ni wenye kuhitaji zaidi ufahamu wa kujua ukubwa na utukufu wa Uislamu kwani ni dini ya usamehevu na wepesi, hakuna kupindisha ndani yake wala kuweka ugumu wala udanganyifu si kwa maneno wala kwa madhumuni.

Ewe Mwenyezi Mungu ihifadhi Misri yetu na uinue bendera yake kwa waja wote.